DAWASA
Dar es Salaam Water Supply & Sanitation Authority
ISO 9001:2015 Certified

# DAWASA YETU

TAREHE: 21 AGOSTI - 28 AGOSTI 2024 | TOLEO NA. 0172

# DAWASA NA TARURA KUENDELEZA USHIRIKIANO ULINZI WA MIUNDOMBINU



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (**DAWASA**) imekutana na kufanya mazungumzo na Wakala wa **Barabara Vijijini** (**TARURA**) Mkoa wa Dar es salaam yaliyolenga kuangalia njia bora ya kushirikiana katika ulinzi na utunzaji wa miundombinu katika **Jiji la Dar es salaam**.

Akiongea katika kikao kazi hicho, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu **DAWASA**, **Mhandisi Mkama Bwire** ameeleza kuwa **TARURA** ni wadau muhimu sana na kwapamoja hushirikiana na **DAWASA** katika utekelezaji wa kazi zao.

"**DAWASA** tupo tayari kushirikiana kwa karibu sana na **TARURA**, tunaomba kipindi cha utekelezaji wa miradi ya **TARURA** hasa ukarabati wa barabara tuweze kupeana taarifa mapema ili kuweza kuondoa miundombinu ya maji na kuzuia uharibifu" ameeleza **Mhandisi Bwire**.

Kwa upande wake Meneja wa **TARURA** Mkoa wa **Dar es salaam** Mhandisi **Geofrey Mkinga** ameishukuru **DAWASA** kwa ushirikiano na kusema kwamba wamejipanga kikamilifu kushirikiana na **DAWASA** katika kutekeleza malengo makuu ya Serikali ya kuwapatia wananchi huduma pamoja na utunzaji wa pamoja wa miundombinu.